**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE**
**SHULE YA SEKONDARI LIWALE**

**S.L.P139**
**LIWALE**
**28/03/2022**

**SIMU:-**
***Mkuu wa shule-0713 943 756 / 0693 392 176***
***Email-----mussamwenda26@gmail.com***
***Makamu mkuu wa shule- 0716 147 690***
***Mtaaluma mwandamizi - 0686 142 921***
***Matron-0624 445 217***
***Patron-0758373015***

**KUMB.NA.LWSS/J.6/VOL.2/2022**

**JINA-----------------------------------------**
**S.L.P--------------------------------------------**

**YAH:KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO 2022**.

1.**Utangulizi**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.
Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga **KIDATO CHA TANO** Julai 2022 katika shule ya sekondari **LIWALE** mkoa Lindi.Masomo kwa muhula wa kwanza yataanza rasmi tarehe………/2022.Wewe unatakiwa kuripoti hapa shuleni kati ya tar….2022 na tayari kwa kuanza masomo tarehe …./2022.

Shule ya sekondari Liwale ipo Liwale mjini km 2 magharibi mwa mji wa Liwale.Shule ni ya mchanganyiko wasichana na wavulana kidato cha kwanza hadi cha sita (1-6).Utakapofika Liwale mjini chukua usafiri wa pikipiki au Bajaji au Tax utalipa kati ya 2000/= na 3000/= hadi kufika shuleni.Kwa wanaotokea au kupitia Dar es salaam,mabasi ya Liwale yanapatikana kituo cha mabasi cha Sudani au Temeke mwisho au kituo cha mabasi Mbagala Rangi tatu.

## 2.Maagizo mbalimbali ya kuzingatia

## I.sare na mavazi ya shule

**WASICHANA**

I. Sketi 2 za rangi ya bluu nzito(dark blue),kitambaa kizito.**SKETI IWE NDEFU** na iwe na upana wa kutosha(**isibane)**
II. Mshono wa sketi uwe wa **rindaboksi.**
III. Mashati mawili meupe,mikono mifupi,kitambaa cha tetroni na yasiwe ya kubana mwili pamoja na skafu ya rangi ya kufanana na sketi.
IV. T-shirt zinapatikana shuleni.

V. **VIATU VYEUSI,VYA NGOZI,VYA KUFUNGA NA KAMBA,VISIWE VYA KUPANDA AU VYA GOROFA AU VYENYE KISIGINO KIREFU**.
VI. Soksi nyeupe jozi/pea 2 au zaidi
VII. Gauni mbili za rangi ya kijani zenye marinda na **yawe marefu**,aina yoyote ya nguo hairuhusiwi kuvaliwa hapa shuleni.
VIII. Nguo za michezo(tracksuit,raba n.krangi ya **bluu**(blue)
IX. Ndala jozi moja
X. Kitenge doti moja( utavaa ukiwa bwenini**)** **1**
XI. Hijabu inaruhusiwa.Endapo utaamua kushona hijabu,utatakiwa kushona sketi ndefu yenye marinda na nusu kanzu.

**WAVULANA**

I. Suruali 2 za rangi ya bluu nzito (**dark blue**)kitambaa kizito na upana wa suruali chini usipungue inchi **16**.(**Tafadhali zingatia ili kuepuka usumbufu**).
II. Mashati 2 meupe,mikono mirefu,kitambaa cha tetroni na yasiwe ya kubana
III. Suruali mbili za rangi ya kijani kwa ajili ya kushindia na kwa ajili ya wakati wa kazi za nje.Aina nyingine yoyote ya nguo hairuhusiwi kuvaliwa hapa shuleni.
IV. Soksi nyeusi jozi/pea 2 au zaidi.
**V. VIATU VYEUSI,VYA NGOZI,VYA KUFUNGA NA KAMBA NA VISIWE VYA KUPANDA AU VYA GOROFA AU VYENYE VISIGINO VIREFU.**
VI. Tai rangi ya kufanana na suruali (dark blue)
VII. T-shirt Zinapatikana shuleni kwa Tshs**.15,000**/=
**VIII. MKANDA MWEUSI WA NGOZI USIO NA PICHA ,UREMBO WALA MAANDISHI.**
IX. Nguo za michezo (raba na track suit rangi nyeusi na jezy za **TANZANIA** za bluu
X. Ndala jozi moja.

***II. UVAAJI WA SARE***

**STAILI ZIFUATAZO ZA UVAAJI WA SARE YA SHULE HAZIRUHUSIWI**

I. Kushusha au kulegeza suruali/kuvaa mlegezo
II. Kuvaa sare ya shule bila kuchomekea shati .
III. Kwa wavulana kuvaa sare bila kuchomekea shati na kufunga mkanda.
IV. Kwa wasichana kuvaa sketi fupi ni kosa
V. Kuvaa viatu bila soksi ni kosa
VI. Kuvaa sare bila tai kwa wavulana au bila skafu kwa wasichana hairuhusiwi
VII. Kuvaa nguo au mavazi yasiyotajwa kwenye maelekezo haya ni kosa.

***MSISITIZO***

***Wazazi na wanafunzi wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kuhusu sare na uvaaji wa sare. Wakati mwingine wanafunzi kwa matakwa yao binafsi huamua kushona sketi fupi au suruali iliyobana na iliyochongolewa .Mavazi ya aina hiyo hayatakubaliwa.*EPUKA USUMBUFU NA KERO MAPEMA.ZINGATIA MAELEKEZO ULIYOPEWA .UTAKAPORUDISHWA KWA SABABU YA KUTOZINGATIA MAAGIZO YALIYOTOLEWA USIJE KULALAMIKA WALA KUMLAUMU MTU YOYOTE.**

### III.*Ada na michango mbalimbali ya shule*.

Tafadhali lipa ada na michango ifuatayo.Lipa kupitia akaunti ya shule[**LIWALE SECONDARY SCHOOL CAPITATION,AKAUNTI NA.70301200045 Benki NMB Tawi Liwale.**

| NA | MCHANGO | MUHULA WA 1 | MUHULA WA 2 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya shule | 70,000/= | - | 70,000/= |
| 2 | Taaluma | 15,000/= | - | 15,000/= |
| 3 | Vibarua wa shule | 20,000/= | - | 20,000/= |
| 4 | Mtihani wa moko | 40,000/= | - | 40,000/= |
| 5 | Fedha ya tahadhari | 5,000/=(haitarejeshwa) | - | 5,000/= |
| 6 | Rimu ya karatasa | 1 | 1 | 2 |
| 7 | Matibabu | 15,000/= | - | 15,000/= |
| 8 | Wino wa fotokopi | 5,000/= | - | 5,000/= |
| 9 | Michezo | 8,000/= | - | 8,000/= |
| 10 | Ukarabati wa samani na majengo | 10,000/= | - | 10,000/= |
| | | **188,000/=** | **-** | **188,000/=** |

**iv.VIFAA VYA KAZI,USAFI,MALAZI NA CHAKULA**

**Unatakiwa kufika na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya kufanyia kazi ndogondogo za nje,chakula na kwa ajili ya malazi**

I. **Jembe (ngwamba)pamoja na mpini**
II. **Panga moja**
III. **Kwanja moja**
IV. **Reki moja**
V. **Fagio ya nje na ya ndani**
VI. **Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko**
VII. **Sahani,bakuli,kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula**
VIII. **Chandarua**
IX. **Godoro futi 2½**
X. **Shuka 2 au zaidi za rangi ya blue bahari (light blue)**
XI. **Sabuni ya maji lita** 1

***v.VIFAA VYA MASOMO***

**I.Vitabu vya masomo ya tahasusi(combination)husika.**
**II.Daftari(counter book)za kutosha kulingana na masomo husika**.

***VI. SHERIA ZA SHULE***
**A.HESHIMA KWA UJUMLA.**

I. **Kila mwanafunzi ni lazima asimame kuamkia kwa mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri.**
II. **Ni kosa kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu ya matusi kashifa au kejeli**
III. **Unatakiwa kukumbia unapoitwa au kutumwa na mwalimu au mtu yeyote .**
IV. **Unatakiwa kuheshimu bendera ya taifa ,wimbo wa taifa ,picha za viongozi wa serikali ,nembo ya taifa n.k.**
V. **Mwanafunzi ni lazima anyoshe mkono na kusimama anapouliza au kujibu swali.**
VI. **Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele darasani na ni kosa kutoka darasani bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa.**

VII. **Mwanafunzi haruhusiwi**
- **Kuvuta sigara**
- **Kugombana**
- **Kugomea adhabu halali ya mwalimu**
- **Kuvaa mavazi yasiyo na heshima au yasiyoruhusiwa ,kuvaa pete,hereni,kofia ,bangili,mkufu.**
- **Kufuga ndevu,nywele ndefu,kucha ndefu wala kunyoa kihuni (kiduku,upara,pank n.k)**
- **Kufanya biashara akiwa shuleni**
- **Kupaka wanja ,dawa ya kicha,dawa ya nywele** **3**
- **Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ya ruhusa**
- **Kuangalia TV ya shule ni kuanzia ijumaa saa 12 jioni hadi jumapili saa 12.00 jioni**
- **Kila mwanafunzi ni LAZIMA ahudhurie maandalizi ya jioni darasani na si bwenini (preparation)kila siku isipokuwa ijumaa na jumamosi.**

VIII. **Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.**

IX. **Unatakiwa kuhudhuria katika kila shughuli ya shule kadiri itakavyopangwa mfano paredi kila siku kwa hali yoyote ile.**

X. **.Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule**

XI. **Kuvaa sare ya shule wakati wote kwa mujibu wa taratibu za shule.**

XII. **Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.**

XIII. **Kutunza mali za umma**

XIV. **Hairuhusiwi mwanafunzi/wanafunzi kufanya au kuendesha au kushiriki mkutano wowote usioendana na ratiba au kalenda ya shule.**

**NB.Kazi mbalimbali za shule ni pamoja na kufagia ,kulima au kufyeka ,kukata kuni,kumwagilia miti,kupanda na kutunza miti ya shule,kuosha vyombo vya chakula ,na nyinginezo ambazo hujitokeza wakati wowote**).

## B. SHERIA ZA BWENI

I. Hairuhusiwi mwanafunzi wa kiume kuingia bweni la wasichana na wanafunzi wa kike kuingia bweni la wavulana.

II. Huruhusiwi kutoka nje ya shule isipokuwa kwa kibali/ruhusa rasmi ya uongozi wa shule.

III. Mwanafunzi wa bweni ni lazima AVAE VIZURI sare ya shule iliyokamilika siku na muda wowote awapo darasani na anapotoka nje ya shule.

IV. Hairuhusiwi kutoa samani yoyote ya darasani(kiti,mezadawati)na kupeleka bwenini.

V. Aina yoyote ya silaha (panga,jembe,kisu,kwanja n.k)haviruhusiwi kuwepo bwenini.

VI. Hairuhusiwi mwanafunzi **KUMILIKI,KUTUMIA /KUWA NA SIMU**shuleni.Mawasiliano au taarifa zozote muhimu baina ya mzazi na motto yapitie kwa mwalimu wa bweni(Angalia namba za simu juu).Kosa la kumiliki na kutumia simu ni kufukuzwa shule.

VII. Ni kosa kwa mwanafunzi kuharibu kwa makusudi au kwa uzembe kifaa au mali ya shule .Uharibifu wa namna hiyo utafidiwa au kulipwa.

VIII. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoa kiti/ meza nje ya darasa kwa matumizi yoyote yale pasipo na kibali.

IX. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie maandalizi ya usiku(Night preparations) kuanzia saa 2.00 – 4.30

X. Ni kosa kwa mwanafunzi kukaa/kulala bwenini wakati vipindi vya darasani vikiendelea(Ni sharti mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote vya darasani)

XI. Kila mwanafunzi wa bweni **NI LAZIMA** ahudhurie paredi ya asubuhi na mchana kila siku bila kukosa.

XII. Kila mwanafunzi wa bwqeni ni lazima kuzingatia kwa vitendo usafi wa bweni na maeneo ya bweni,jiko na maeneo yote ya shule.

XIII. Mwanafunzi wa bweni haruhusiwi kupika chakula chake mwenyewe au cha shule

XIV. Ni kosa kwa mwanafunzi kuitisha ,kuendesha ,kushiriki kikao /mkutano isipokuwa kwa kibali cha mkuu wa shule au kwa mujibu wa kalenda ya shule.

XV. Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha kwa namna yoyote ile na harakati za kisiasa awapo hapa shuleni.

XVI. Mwanafunzi yoyote anapougua ni lazima atoe taarifa kwanza kwa kiongozi wa bweni /mwalimu wa bweni.

XVII. Ni kosa kwa mwanafunzi kudharau bendera ya taifa ,picha za viongozi wa taifa,nembo ya taifa,wimbo wa taifa na fedha za taifa.

**Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea au kuingia sehemu zifuatazo**:

- Chumba cha mwalimu/walimu.(ofisi)
- Nyumba ya mwalimu
- Vilabu vya pombe
- Majumba ya starehe
- Nyumba za kulala wageni [Guest House]

**C.KUFUKUZWA SHULE**

Makosa yafuatayo yanasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule:

1. Wizi 2. Ubakaji/Ushoga 3. Utoro wa muda mrefu 4. Makosa ya jinai
5. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo bangi na nyinginezo.

6.kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7.kupigana au kumpiga mwenzako
8.kudharau bendera ya taifa
9.kuolewa au kuoa
10.kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11.kutoa mimba
12.kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama shuleni
13.kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu au kiongozi
14. kujificha porini kwa lengo la kutoroka vipindi au shule kwa ujumla
15.kuwa na **SIMU YA MKONONI**

…………………………
**MUSSA O. MWENDA**
**MKUU WA SHULE**

**VIAMBATISHO**

1.Fomu ya vipimo vya hospitali(Medical Examination Form)
2.Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi
3. fomu ya taarifa za mzazi/mlezi

**FOMU NAMBA 1.**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**LIWALE SECONDARY SCHOOL**
**P O BOX 139**
**LIWALE.**
**20/5/2021**

**TO THE MEDICAL OFFICER**
**………………………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………..**

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION
TO**……………………………………………………………….…(Name in full)**

**Please may you examine the above named pupil and give us the report regarding his /her physical and mental fitness/unfitness for undertaking secondary school studies and other school activities in general.**

1. **Eye Test………………………………………..……………………………………………….**
2. **Hears test……….……………………………..…….…………………………………………….**
3. **T.B Test………………………………………..………………………………………………….**
4. **Pregnancy (For girls) ………………………….....………………………………………………….**
5. **Abdomen……….………………………..…..…….……………………………………………….**
6. **Chest test………………………………………………..…………………………………………….**
7. **Stool test……………………………………………………………………………………………**
8. **Urine examination……………………..…………………………………………………….**
9. **Stool……………………….………………………………………………………………….**
10. **Spleen…………………..…………………………………………………………………..….**

**ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g Physical defects or impairment, infection, family diseases etc…...………………………………………………………………………………………………**
**………………………………………………………………………………………………………**
**………………………………………………………………………………………………………**
**………………**

**I certify that, the above named pupil is suitable/unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons:**

**………………………………………………………………………………………………………**
**………………………………………………………………………………………………………**
**…………………………………………………………………………………………………….**

**Name of Medical Officer :……………………….……………………………Signature……………**

**Date :………………………………………    Official Stamp……………………….**

**FOMU NAMBA2.**

**: TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1.Mkoa……………………………..………………Wilaya :…………………………………………..

2. Tarafa…………………………………………………..Kata: ………………………………………..

3. Mtaa/ Kijiji …………………………………………..

4. Michezo anayopendelea.

| Na | Jina la Mchezo |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |

5. Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika

| Na | Aina ya uongozi | Shule | Mwaka |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |

Mimi( Jina la mwanafunzi)…………………………………………………………nakubali/sikubali nafasi hii ya kujiunga na elimu ya sekondari katika shule ya sekondari ya LIWALE.

Naahidi kuwa,wakati wote wa uwanafunzi wangu hapa shuleni nitakuwa mtiifu na nitafuata sheria za shule kama zilivyoelekezwa.

Naahidi kuwa sitashiriki katika migomo ya aina yoyote ile hapa shuleni,wala fujo za aina yoyote,wala kutenda makosa yoyote ya jinai

Saini ya mwanafunzi……………………………........Tarehe……………………

**FOMU NAMBA 3.**

**TAARIFA ZA MZAZI/ MLEZI**

1. JINA KAMILI LA MZAZI/ MLEZI…………………………………………………………………
2. KAZI:…………………………………………..
3. ANUANI…………………………………NAMBA ZA SIMU:……………………………………
4. MKOA:…………………………..WILAYA:………………………TARAFA:…………………
5. KATA:…………………………………..MTAA/KIJIJI……………………………………………
……
6. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo

| Na | JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |

Mimi Mzazi/ Mlezi wa ……………………………………………………………...ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa shule ya sekondari LIWALE katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokua shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sharia, kanuni na taratibu za shule. Pia, nitakua tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makossa atakayofanya.

Jina…….……………………………………Saini…………………………Tarehe…………………..